Mwanzo Na Mwisho Wa Kipindi Cha Mataifa

Habari za jioni, marafiki. Ninashukuru sana kuwa hapa, usiku wa leo, tena. Ndiyo kwanza niondoke hapa, muda mfupi uliopita. Nadhani, nilitoka karibu saa kumi. Na kisha ilinibidi . . . tulishuka kuwaona marafiki wengine zaidi. Kisha nikarudi, saa moja na dakika tano, ilibidi tu nirudi huku chini. Kwa hiyo kwa namna fulani inanibidi kutafuta somo, bado, Ndugu Neville.

2 Lakini, sasa, kuna haja ambayo imetumwa hivi punde, kutoka kwa mtu fulani huko Chattanooga, Tennessee, mpendwa ambaye alikuwa katika ajali majuma matatu yaliyopita, na angali amepoteza fahamu, bado. Naye anahitaji maombi hapa, kutoka kanisani. Na . . .

3 [Ndugu Neville anasema, "Ndugu Bill?"—Mh.] Naam, ndugu? ["Je, naweza kufanya tangazo?"] Hakika unaweza. Ndugu Neville, njoo tu. ["Kunradhi, Ndugu Bill."] Naam, bwana. ["Karibu nisahau. Nilitoa ahadi ya kufanya tangazo usiku wa leo." Sehemu tupu kwenye kanda.]

4 Tulikuwa—tulikuwa tukizungumza juu ya Melkizedeki, kwamba Yeye alikuwa ni Nani, wala hata hatukukaribia kumaliza hilo. Lakini labda, wakati mwingine nikirudi humu, tunaweza kuendelea kuanzia hapo, bado katika Kitabu cha Waebrania.

5 Lakini, usiku wa leo, tufungue kwenye Kitabu cha Danieli. Nanyi mlio na Biblia zenu, fungueni Danieli 12. Nasi tutasoma kidogo kutoka humo, na kuzungumza, labda, juu ya baadhi ya Neno la Mungu kutoka kwenye Kitabu cha Danieli.

6 Sasa, Danieli alikuwa mmoja wa . . . alikuwa nabii aliyetekwa nyara kutoka Yerusalemu, akapelekwa Babeli, katika uhamisho wa Babeli, na Mfalme Nebukadreza. Alikuwa jamaa mdogo aliposhuka kwenda Babeli. Hakukuwako na wengi wao ambao walikuwa bado wameshikilia ile imani kuu ya kale.

7 Nampenda Danieli, kwa sababu ninii yake . . . alikuwa amekusudia hilo moyoni mwake, aliposhuka kwenda Babeli, kwamba atadumu mwaminio, wala hangejitia najisi kwa vyakula vya mfalme, na kadhalika. Sasa, jambo lile lile . . .

8 Naye Danieli alikuwa nabii kwa Mataifa. Danieli aliuona wakati wote wa Mataifa ukipanda na kushuka. Alikuwa wa kwanza kuwa, tunachoita, nabii wa Mataifa. Yeye hakuwa Mmataifa, yeye mwenyewe. Lakini alikiona kipindi cha wakati

wa Mataifa, tangu mwanzo hadi mwisho; katika kichwa cha dhahabu, na kuishia katika miguu ya chuma na udongo.

9 Na wakati akiwa huko chini, aliazimu moyoni mwake kwamba hatajitia najisi kwa vyakula vya mfalme, wala shughuli za mfalme.

10 Pia kundi lingine la ndugu, walioitwa Shadraka, Meshaki na Abednego, lilikuwako kule chini pamoja nao; ambao hawakuwa manabii, bali waaminio. Nao, pia, waliazimu moyoni mwao. Ndipo basi wakati hao waaminio wanne walipokutana pamoja, ningewazia mara nyingi sana, walikuwa na mikutano ya maombi ya pamoja.

11 Kama tu tufanyavyo, tunakusanyika kwa sababu tuna vitu shirika. Unajua, kuna msemo wa kale unaosema, "Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba," na hiyo ni, ni methali ya kale, hasa, na hilo ni jambo zuri sana, pia. Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba. Je, hamfurahii hilo? Hakika. Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba.

12 Si muda mrefu uliopita, nilikuwa nimeketi katika mkutano ambapo kulikuwa na mtu akijadili jambo fulani. Naye akasema, "Vema . . ." alikuwa akizungumza juu ya nafsi zilizoenda kifungoni, zilizokuwa kifungoni, ambao Yesu aliwaendea na kuwahubiri, baada ya kifo Chake. Basi mtu huyu aliyekuwa akizungumza, alisema, "Vema, mwaonaje kuhusu hilo?"

13 Ndipo ndugu mmoja mweusi akasimama. Akasema, "Vema, hivyo ndivyo tu Biblia ilivyosema. 'Alienda akawahubiri nafsi zilizokuwa kifungoni.'"

Kasema, "Unafikiri ilikuwa ni nini?"

14 Kasema, "Ilikuwa ni 'Nafsi zisizotubu, katika uvumilivu, katika siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa,' kama tu vile Biblia ilivyosema."

15 Akasema, "La." Kasema, "Hilo ni kanisa hili, likiwahubiri wale Wapentekoste walio katika madhehebu haya na kila kitu, likiwatoa kifungoni."

16 Akasema, "Sasa, angalia hapa, ndugu," akasema, "Pentekoste hata haikutajwa hapo." Akasema, kwamba, "Alisema tu, kwamba, 'Alienda akawahubiri nafsi zilizokuwa kifungoni.'"

Kwa hiyo nikasema, "Amina. Hiyo ni kweli."

17 Ndipo huyo mhudumu akageuka akaniangalia, na kusema, "Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba."

18 Nikasema, "Hiyo ni kweli, ndugu wa Imani moja ya thamani, wakiamini kile tu ambacho Maandiko yanasema ni Kweli."

Danieli alikuwa na watatu wa hao wenzake waliokuwa pamoja naye.

19 Unajua, ni vizuri, unapokuwa mbali na nyumbani, kupata mtu ambaye yuko pamoja nawe, mtu ambaye atakutetea, rafiki mwema kabisa. Loo, jamani! Katika nchi za kigeni, ukimpata mtu anayetaka kuwa rafiki yako, na anakupenda na kukutetea, huyo ana thamani kubwa sana; hasa sana mgeni.

Basi hawa ndugu walichukuliwa mateka kutoka mjini mwao.

20 Nao mji wao ukateketezwa. Na vyombo vyao vyote, na vitu vitakatifu vya Mungu, vilihamishwa mpaka Babeli, na kuwekwa katika nyumba ya hazina ya Mfalme Nebukadreza, ambaye alikuwa amewahamisha mpaka huko chini, mfalme mkuu, mashuhuri wa Mataifa. Sasa, kama—kama Mungu ameruhusu hilo, mji wao uchomwe moto, kanisa lao lichomwe moto, na kuwashusha mpaka mjini, ilikuwa ni kwa sababu walikuwa wamemwacha Mungu.

21 Lakini bado alikuwa na mwaminio ambaye angeweza kuweka mikono Yake juu yake, na kusema, "Huyu ni mtumishi Wangu."

22 Mungu daima amekuwa na shahidi, mahali fulani. Kamwe hajiachi bila shahidi. Haidhuru, pengine amesalia mmoja peke yake, bali Yeye daima amekuwa na mtu ambaye angeweza kumwekea mikono Yake, na kusema, "Huyu ni mtumishi Wangu, na atafanya vile ninavyomwambia." Sasa, tunapenda hilo.

23 Tunaona basi, ya kwamba, wakati ndugu hawa walipokuwa kule chini, waliwekwa kwenye majaribu.

24 Mfano mzuri sana wa pale mwaminio wa kweli anapofikia anapomkubali Bwana Yesu kama Mwokozi wake kweli. Daima yeye hutiwa majaribuni. Shetani angali yuko kwenye shughuli ya majaribu. Nayo yanatokea tu yapate kukusaidia. Ni kwa manufaa yako.

25 "Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa, kurudiwa, kupigwa mijeledi," kwa maneno mengine, "kutwangwa kidogo, kunyoosha. Na kama Mungu akitupa adhabu, wala hatuwezi kuistahimili, basi tunakuwa watoto haramu, wala si watoto wa Mungu."

26 Sasa, mtu ambaye kweli ameuelekeza uso wake Mbinguni, haidhuru ni nini kinachotukia hapa duniani, bado ameuelekeza uso wake Mbinguni. Marafiki zake wanaweza kumwacha. Familia yake inaweza kumwacha. Mchungaji wake anaweza kumwacha. Lakini kuna Mmoja ambaye hatamwacha; huyo ni Mungu. Na wakati umekata shauri! Napenda hilo.

27 Danieli alikuwa ameteketeza madaraja yote nyuma yake. Hakuwa na mpango wa kurudi nyuma, tena. Hakuwa akiangalia njia yake ya kurudi nyuma. Alikuwa akitazama, akiyaacha yale mambo yaliyopita. Alikaza mwendo aifikie mede ya wito

mkuu. Hilo ndilo tunalopaswa kufanya. Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa likifanya.

28 Na kama ninavyoona, basi, Mungu alimruhusu Shetani kumpa jaribio. Na, loo, waliwajaribu, kwa moto. Waliwajaribu, pia, penye tundu la simba. Na kila wakati, Mungu aliwatoa, zaidi ya washindi.

29 "Majaribu ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya nayo yote." Hiyo ni ajabu jinsi gani! Jinsi tunavyothamini hilo. Majaribu, dhiki, majaribio, yote yakifanya kazi kwa manufaa! Baada ya muda, Mungu anaweza kuona kwamba anaweza kuweka tumaini Lake kwako, ndipo basi atakufanyia mambo makuu.

30 Sasa tunaona, basi, ya kwamba Danieli alifanyika chombo mkononi mwa Mungu, alipokuwa mbali na watu wake mwenyewe, nje ya mji wake mwenyewe, mbali na kanisa lake mwenyewe, katika nchi ya kigeni, Mungu alimtumia.

31 Sasa, unaweza kuwa mbali na chochote unachoweza kuwa. Unaweza kuwa mbali na wapendwa wako wote, au unaweza kuwa mbali na kanisa lako, lakini bado unaweza kuwa chombo mikononi mwa Mungu. Mungu anaweza kukutumia kwa ushuhuda au kwa kitu chochote anachotaka kukutumia.

32 Mifano mizuri! Biblia imejaa tu mambo hayo, kila mahali unapogeukia. Hivi hampendi kulisoma Neno? Loo, mimi hulisoma tu, wakati mwingine, na kulia.

33 Hapa siku chache zilizopita, nilikuwa nikisoma chumbani mle, ndipo ikanibidi tu kuketi chini na kulia kama mtoto mchanga. Nilisimama na kutembea kukizunguka kiti changu, nikaweka mkono wangu juu ya kiti changu, nikaitazama Biblia yangu tena; nikaangua tu kilio. Nikakizunguka hicho kiti tena, nikaitazama tena. Nikawazia, "Ee Mungu, mle ndani kuna Uzima wa Milele, kwa kila mwanamume ama wanawake watakaojasiria kuweka tumaini lao ndani Yake, na kuiamini." Uzima wa Milele!

34 Naye alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Yachunguzeni Maandiko.

35 "Neno la Mungu ni taa ya miguu yetu," ambalo—ambalo tunapaswa kuongozewa, basi. Ni Mwanga unaofuata njia inayotuongoza kutoka ushindi mmoja hadi mwingine.

36 Sasa, kabla hujaweza kuwa na ushindi, inabidi kuwe na vita. Na kama hakuna vita, hakuna ushindi. Kwa hivyo tunapaswa kushukuru kwa ajili ya vita na majaribu, na ni Mungu akitupa nafasi ya kupata ushindi. Loo, jamani! Je, hilo halikufanyi kuwa bora zaidi kidogo sasa? Unaona? Vita vinakuja; mtu fulani akisema jambo baya juu yako; ugonjwa unakujia. Labda Mungu anakupa hayo mateso mepesi, ili aweze kukuponya na

kukuonyesha fadhili Zake, akuonyeshe anachomaanisha kwa jambo hilo, anakupenda.

37 Ile hadithi ya kale ya mchungaji iliyosimuliwa kule Yerusalemu, katika nchi takatifu, ya mchungaji, aliyekuwa amembeba ko—kondoo. Naye akasema, "Unambeba kwa sababu gani?"

Kasema, "Amevunjika mguu."

Kasema, "Ilikuwaje; kaanguka kutoka mwambani?"

Kasema, "Hapana. Nilimvunja mguu."

38 Akasema, "Mbona, wewe ni mchungaji katili, kumvunja mguu huyo kondoo."

39 Kasema, "Hapana. Nilimpenda." Kisha kasema, "Alikuwa anaenda kombo, wala nisingeweza kumfanya anijali. Kwa hiyo, nikauvunja mguu wake, nipate kumpa uangalizi wa ziada, ndipo basi anipende na kunifuata."

40 Wakati mwingine, Mungu hana budi kuacha afya yetu izorote, kidogo tu, apate kutupa uangalizi wa ziada, kutuweka pajani Mwake, kutubembelezea kifuani Mwake. Daktari aliposema hakuna liwezalo kufanywa; basi anatuweka kifuani Mwake, anasema, "Unaona, ninakupenda. Naenda kukupa afya." Unaona? Loo, hilo si hufanya maisha kuwa bora zaidi kidogo? Loo, Yeye ni mkuu sana! Yeye ni Mchungaji wa ajabu. Sivyo?

41 Si ajabu Daudi alisema, "Bwana ndiye mchungaji wangu. Sitapungukiwa na kitu." Na jinsi anavyotuongoza kando ya maji matulivu; na kuzihuisha nafsi zao; na kuvifurikisha vikombe vyetu; na—na kututia mafuta mbele ya adui! Je, uliwahi kupakwa mafuta mbele ya adui yako? Kushuhudia tu mpaka kikombe chako kikafurika tu, unajua. Ni ajabu jinsi gani kutiwa mafuta mbele ya adui yako!

42 Sasa angalia, basi, Mungu alimchukua Mfalme Nebukadreza na kumfanya chombo mkononi Mwake. Ndipo Mfalme Nebukadreza alipokufa, akiisha kuninii. . .Nyasi zilimea; nywele zake, kama simba, au kama manyoya ya tai; na makucha ya vidole vyake kama kucha za tai, na kadhalika. Naye Mungu ilimbidi amfahamishe ni Nani aliyekuwa Mfalme halisi.

43 Baada ya kifo chake, Belshaza, mjukuu wake, alimrithi. Halafu, basi, alikuwa katili kuliko Mfalme Nebukadreza. Ndipo usiku mmoja, pale, walikuwa na karamu kubwa mno. Wakawaita mahakimu wao—wao wote na maafisa wao wote ndani, kwa hafla kubwa mno. Basi wakati walipokuwa wakifanya hafla hii, nao walikuwa. . .wakaenda, wakaitana, kisha wakavitwaa vile vyombo, vyombo vitakatifu vya Mungu; ili tu kumdhihaki Mungu, na kuinywea miungu yao divai, kutakiana heri, kwa vyombo vya Bwana.

44 Sasa, mtu anaruhusiwa kusafiri umbali fulani, lakini kuna mstari wa utengano kati ya Uzima na mauti. Kamwe usiuvuke huo. Unaona? Unaweza kuendelea na maskini upumbavu wako kwa muda, lakini afadhali ujue mahali huo mstari ulipo. Je, Bwana aliwahi kukuhadharisha na jambo lolote? Yeye hufanya hivyo, kwetu sote, anavuta hatamu za kuhadharisha, anasema "Usipite hapo sasa." Basi afadhali uangalie unachofanya, tangu hapo na kuendelea, ikiwa unaelekea kwenye mstari huo.

45 Basi usiku huo, wakati Mungu alipovuta hatamu za kutahadharisha juu yake, wala asingesikiliza. Anashuka na kuvitoa vyombo vya Bwana, anaanza kunywa divai, na pongezi kwa mungu wao. Ndipo mkono ukashuka kutoka Mbinguni, ukaandika ukutani, "MENE, MENE, TEKELI, NA PERESI." Maana yake, "Umepimwa katika mizani, nawe umeonekana kuwa umepungukiwa." Hakuna aliyeweza kuyafasiri. Yalikuwa ni lugha zisizojulikana.

46 Basi palikuwa na mtu pale, aliyekuwa na karama ya kufasiri, Danieli, kwa hiyo akashuka na kufasiri na kumwambia mfalme kile ambacho kitatukia. Basi, hapo, Mungu akaliangamiza taifa hilo, Babeli.

47 Wakati, Danieli, alipokuwa huko, aliona maono makubwa, akaandika habari zake, kwa ajili ya faraja hii kuu tuliyo nayo leo, akijua, na kuweka katika utaratibu, mwisho wa ufalme wa Mataifa.

48 Angalieni jinsi lilivyo kamilifu. Lipateni tu kwa makini sasa. Aliona, kwanza, ile sanamu imesimama kondeni, wakati alipofasiri ile ndoto ya mfalme.

49 Alikuwa mtu wa kiroho. Aliota ndoto, aliona maono, alifasiri ndoto. Mungu alikuwa pamoja naye, na kila mtu alijua hilo, pia.

50 Naye alipoona lile ono, kichwa cha dhahabu, na kifua hapa cha fedha, na mapaja ya shaba, na miguu ya chuma, angalieni, kila ufalme ulizidi kuwa mgumu zaidi. Ufalme wa Mfalme Nebukadreza ulikuwa kichwa cha dhahabu. Aliifasiri, akamwambia jinsi hasa falme hizo zingefuatana hadi mwisho. Ndipo angalieni, kutoka kwa dhahabu, ndiyo laini kuliko zote, fedha inafuata, halafu shaba, kisha chuma kinafuata; ngumu zaidi, ngumu zaidi, baridi zaidi, mbali zaidi!

51 Angalieni, basi, katikati ya hayo yote, Danieli aliitazama hiyo sanamu hata Jiwe likachongwa mlimani, ambalo lilichongwa bila kazi ya mikono. Likabiringika kwenye hiyo sanamu na kuivunja, na kuifanya kama ngano ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari, na pepo zikaipeperusha. "Nalo hilo Jiwe likakua likawa mlima mkubwa ukaijaza dunia yote na bahari." Huko kulikuwa ni kule Kuja kwa Bwana Yesu, ambako sasa kumekaribia.

52 Anaendelea. Alipokuwa kule chini ukingoni mwa mto, siku moja, aliingia katika njozi kisha akaona ono. Wengi wa wale

waliokuwa pamoja naye, hawakuona hilo ono, kwa maana lilipewa Danieli pekee. Mnaliona?

53 Mtu anaweza kusimama papo hapo karibu nawe, na kuona vitu ambavyo huwezi kuona, kuyaokoa maisha yako. Hiyo ni kweli. Mtu fulani alisema, “Siamini hilo. Kamwe sikuona chochote.” Kwa sababu halikuwa kwako kuliona.

54 Wale walioandamana na Paulo, wakati Paulo alipobwagwa chini ya farasi wake na ikabidi aanguke mavumbini; na kugaagaa, tuseme, mavumbini; hakuna hata mmoja wao aliyesikia sauti hiyo wala kuona ono hilo. Paulo aliliona.

55 Hakuna hata mmoja wao aliyeiona ile nyota iliyovuka ninii . . . kila mnara wa kuchunguzia, ila wale mamajusi.

56 Mambo mengi, kwa njia hiyo, Mungu amewateua watu fulani waone, na wengine hawawezi kuona. Loo, napenda hilo! Wakati Mungu, katika hekima Yake isiyo na kikomo, amekusudia tangu zamani, au kuagiza awali, mambo fulani kutokea, yanaweza kutokea kwa mtu anayeketi karibu nawe, na wewe hutajua chochote kuyahusu.

57 Angalieni huko Dothani, wakati Eliya alipokuwa huko chini Dothani na wote walikuwa wamezingirwa huko na—na wageni walioingia, jeshi la Shamu; wakimtafuta Eliya, nabii. Kwa maana wakati, walipoanza kugundua, kila wakati Washami walipokuja Israeli, kufanya vita, mbona, Waisraeli wangekuwa tayari kuwavizia.

58 Basi mfalme wa Shamu akawaita, akasema, “Sasa, ngojeni kidogo. Ni nani aliye upande wetu, na ni nani aliye upande wa Israeli?” Kasema, “Mtu fulani katika kundi langu ni jasusi, ambaye atawaambia Israeli mahali tunapoingilia, kwa maana wao sikuzote wako pale wakitungojea.”

59 Basi mtu mmoja alikuwa na ufahamu kidogo wa kiroho juu yake. Akasema, “Hapana, baba yangu. Lakini ni nabii Eliya, kwa maana anajua, kwenye chumba chake cha kulala, hatua nyingine utakayochukua.” Amina.

60 Loo, wakati nguvu za atomiki zitakapoanza kutikisa, nina furaha sana kwamba Neno la Mungu limetwambia mahali pa kwenda. Kimbilieni kwenye Mwamba, Kristo Yesu! Kila mtu ndani Yake yuko salama salmini. Hakuna kinachoweza kukudhuru. Hakuna mabomu ya atomiki, hakuna kobalti, hakuna kitu kingine, kinachoweza kuwagusa waliohifadhiwa na Mungu; salama, salmini, wametia nanga. Ni tumaini zuri jinsi gani tulilo nalo katika Kristo Yesu!

61 Angalieni, palikuwa na mtu mmoja pamoja naye. Mtumishi wake, mvulana wa kiroho, aliendа akamwaga maji mikononi mwa nabii huyo, alikuwa na cheo kikubwa. Lakini alipoona je—jeshi la Washami likizunguka Dothani, walikuwa wameizingira

kabisa, alisema, “Baba yangu, angalia huko nje! Ni idadi kubwa jinsi gani! Kumbe, tumezingirwa!”

62 Sasa, hiyo ni ya kawaida, wakati kila kitu kinaonekana kwenda mrama; wakikunyooshea kidole, wakisema *hivi* na *vile;* naye daktari anasema huwezi kupata afya, na kadhalika. Hilo ni jambo la kawaida tu, kwako kuwazia, “Loo, jamani, huu ndio mwisho!”

63 Lakini Eliya alisema, “Walio pamoja nasi ni wengi kuliko walio pamoja nao.”

64 Sasa unaweza kuwazia jinsi nabii huyo, au huyo Gehazi alivyojisikia, huyo mtumishi. Alimtazama. Akasema, “Mbona, sioni mtu yeyote.”

Akasema, “Mungu, yafumbue macho ya mvulana huyu.”

65 Na mara tu Mungu alipofanya jambo! Hili hapa. Lipateni. Mungu alipoyafungua macho yake ya kiroho; kote huko, yule nabii, yalisimama magari ya Moto na Malaika wa Moto. Mbona, aliona . . . Mbona, magari ya Moto yalilizidi jeshi hilo la Washami, kwa maelfu. Milima ilikuwa inawaka Moto; Malaika wa Moto, farasi wa Moto, magari ya Moto.

66 Na Biblia ilisema, “Malaika wa Mungu hufanya kituo kuwazunguka wale wamchao.”

67 Ni vile vile tu usiku wa leo! Nashangaa ingekuwaje kama mtu hapa, usiku wa leo, alikuwa na uwezo wa kuyapiga macho yako, na kusema, “Angalia, waliosimama kuizunguka maskani hii usiku wa leo!” Ungekuwa mfuasi hapa maisha yako yote. Hakika. Naam, bwana.

68 Wakati mwingine huwezi kuliona Hilo kwa macho yako ya kawaida, bali unaweza kuhisi msukumo Wake, Kitu fulani kilicho karibu. Hisi ya sita inayoonyesha Kitu fulani kiko karibu.

69 Mwangalie Yeye, asubuhi ya leo, akiwafungua masikio viziwi, akiwafanya vilema wa polio watembee hapa, kana kwamba hawana kasoro. Ni kitu gani? Ni hisi ya ndani. Namaanisha, ile hisi, ile hisi ya sita inayofahamu, roho, kwamba kitu Fulani kiko karibu. Mwaminini Mungu!

70 Sasa, hawakuona, yeye hakuona Hilo, kwanza. Lakini, Eliya labda hakuliona, bali aliomba macho ya mvulana huyo yalione. Lakini Elisha alijua kwamba walikuwa pale. Amina.

Tomaso, wakati mmoja, alisema, “Acha nitie mikono yangu ubavuni Mwake.”

71 Yesu akasema, “Sasa unaona na kuamini. Thawabu yao ni kubwa jinsi gani kwa wale ambao hawajaona bado, na hata hivyo wanaamini.” Hao ni sisi usiku wa leo, kwa yeyote atakayeamini, bila kuona.

72 Basi angalieni. Ndipo Eliya akatoka akaenda pale mahali hali hii ya mambo ilipokuwa, naye akawaambia. . . Kwanza, alitoka akaenda huko nje, nayo Biblia ilisema, "Akawapofusha." Vipofu; kisha akawaendea moja kwa moja. Kila mmoja alikuwa na macho makamilifu, nijuavyo mimi. Lakini Maandiko yalisema, "Walikuwa vipofu."

73 Maskini jamaa mmoja, siku chache zilizopita usiku, aliniambia, "Ikiwa wewe ni mtu wa Mungu, nipofushe."

Nikasema, "Tayari wewe ni kipofu." Mnaona? Mnaona? Tayari kipofu!

74 Angalieni. Naye akatoka akaenda kule, mahali ambapo hali hii kuu ya mambo ilipokuwa, jambo hili kuu lilipokuwa. Naye akasema, "Mnamtafuta Eliya?"

Kasema, "Naam."

75 Kasema, "Hima, nifuateni. Nitawapeleka moja kwa moja kwake." Eliya akawaambia hivyo. Walikuwa vipofu juu ya nini? Walikuwa vipofu kwa ukweli kwamba huyo alikuwa ni nabii wa Mungu. Walikuwa vipofu kwake. Naye akawaongoza moja kwa moja hadi kwenye mavizio, tena. Kasema, "Njoni, nitawaonyesha Eliya," na ilikuwa ni Eliya akiwapeleka kule chini.

76 Basi walipoangalia pande zote, na wakakuta kwamba walikuwa wamezingirwa, pande zote. Mfalme akasema, "Baba yangu, yanipasa kuwapiga?"

77 Akasema, "Kwani unaweza kumchukua mfungwa ukampiga?" Kasema, "Wape chakula, na uwarudishe nchini mwao."

78 Hiyo ndiyo njia ya kumaliza vita. Si ni kweli? Bila shaka. Loo, jamani! Laiti tungeichukua tu kanuni hiyo, siku hizi, kumlisha adui yako. "Watendeeni mema wale wanaowatenda mabaya." Amina.

79 Hapo, sasa, upofu.

80 Sasa, Eliya, ama ninamaanisha, si Eliya sasa, bali Danieli: Danieli alitangulia kuona; yeye alikuwa ni nabii; aliona kuja kwa Bwana; aliona wakati wa mwisho ukija; aliwaona Mataifa wakianza.

81 Na kama ukiangalia, Mataifa walianza na i—ibada ya sanamu. Walikuwa wakiabudu sanamu kubwa iliyowekwa huko nje kondeni, sanamu ya mtu: Ninaamini, ya Danieli, mwenyewe. Maana, Mfalme Nebukadreza alikuwa amemwita "Belteshaza," ambaye alikuwa ni mungu wake, naye akaanza kuabudu sanamu ya mtu mwenye haki, mtakatifu. Naye Danieli akakataa kufanya hivyo; ka—kadhalika na wale wana wa Kiebrania, Shadraka, Meshaki, na Abednego.

82 Hivyo ndivyo ulivyoanza. Nao ulihukumiwa; kichwa kile cha dhahabu kiliwasilishwa kwa ibada ya sanamu, wakalazimishwa kwake, na kuishia kwenye Mkono wa kimbinguni ukiandika lugha ya kimbinguni, ambayo ufahamu wa kimbinguni ndio tu ungeweza kuielewa. Amina.

83 Hivyo ndivyo ufalme wa Mataifa ulivyoingia, nao utaondoka vivyo hivyo, hiyo ni kweli, kwa kazi za kimbinguni, tafsiri za kimbinguni. Mnajua ninachozungumzia. Utendaji wa kimbinguni, loo, ajabu jinsi gani! Hivi hamna furaha, usiku wa leo, mnaamini katika mambo ya kimbinguni? Naam.

84 Sasa, basi, baada ya maono haya, Yeye alimwonyesha mahali hasa ambapo mataifa yangekuwa yamesimama. Alimwonyesha jinsi ambavyo miaka mingi bado ilikusudiwa Wayahudi. Akasema, "Masihi atakuja. Atatoa unabii katika majuma sabini, ambalo ni miaka mitatu na nusu. Katikati yake, Yeye atakatiliwa mbali, ambayo ni miaka saba. Majuma sabini yameamriwa kwa ajili ya watu wako; miaka saba ya unabii kwa Wayahudi." Akasema, "Naye Masihi, yule Mtawala, atakuja na kutabiri, katikati ya yale majuma saba, siku saba, atakatiliwa mbali. Katika chukizo, la uharibifu, litasimama mahali Pake. Nao watazikanyaga kuta za Yerusalemu, Mataifa, kwa wakati, wakati, na mgawanyiko wa wakati."

85 Sasa, alipokuja Masihi, Yesu, Yeye alihubiri miaka mitatu na nusu kamili, na akakatiliwa mbali, kwa ajili ya Dhabihu. Dhabihu ya kila siku iliondolewa. Ndipo uharibifu, chukizo la uharibifu, ule uislamu wa Omar, umesimama leo hii mahali pa hekalu takatifu. Msikiti wa Omar umesimama ambapo hekalu lilisimama hasa.

86 Naye akasema, kwamba, "Wangezikanyaga kuta za Yerusalemu, juu ya Yerusalemu, mpaka kipindi cha wakati wa Mataifa kitakapotimia. Lakini, mwishoni mwa Mataifa, bado ingesalia miaka mitatu na nusu, hata hivyo, kwa Wayahudi."

87 Sasa angalieni moja ya mambo ya kushangaza sana katika historia ya kinabii.

88 Sidai kujua unabii wa Biblia. Lakini hii ni kama kusoma gazeti; dhahiri zaidi. Na, tunayosoma Hapa, tunajua ni Kweli.

89 Angalieni, miaka elfu mbili, naam, miaka elfu mbili na mia tano, Wayahudi wametawanyika katika kila taifa chini ya Mbingu. Mungu aliufanya mgumu moyo wa Farao, akawarudisha; aliufanya mgumu moyo wa Hitler, moyo wa Mussolini, na kadhalika, mpaka amewarudisha Palestina. Wakirudi, wamewafanya kuwa taifa tena. Na mnamo Mei sita, 1947, bendera ya Kiyahudi ilipandishwa juu ya Israeli, kwa mara ya kwanza katika miaka elfu mbili mia tano. Bendera ya kale zaidi ulimwenguni ilipandishwa kwa mara ya kwanza baada ya miaka elfu mbili mia tano. Naye alisema, katika siku za mwisho,

"Angeipandisha bendera juu ya Yerusalemu," ikionyesha ya kwamba wakati umekaribia.

90 Basi angalieni, hapa si muda mrefu uliopita, niliona filamu ya kinabii ikichezwa kutoka kule. Nao wanawaleta hao Wayahudi, kwa maelfu, kwa ndege. Mmeyaona kwenye gazeti, na kadhalika. Magazeti ya *Look* na *Life* yamekuwa yakiyatangaza. Maelfu ya Wayahudi wanarudi! Ndipo wakawauliza, wakasema, "Kwa nini mnarudi?" Wazee, vilema, wakiwabeba migongoni mwao, watoto wao walikuwa wakiwabeba. Kasema, "Kwani mnarudi nyumbani mpate kufa?"

Kasema, "Hapana. Tunarudi kumwona Masihi."

91 Yesu alisema, "Mtakapouona mtini ukichipusha majani yake, na miti mingine yote ikichipusha majani yake, jueni ya kwamba wakati umekaribia, ama wakati wa kuchipua umekaribia, wa mavuno. Kwa hiyo, mtakapoona mambo haya yakitukia, inueni vichwa vyenu, ukombozi wenu umekaribia."

92 Usiku wa leo, wakati ulimwengu huu umegubikwa na ukomunisti! Loo, nilikuwa nikizungumza na mtu fulani muda mfupi uliopita, kwenye. . . mmoja wa wataalamu bora sana, ninaamini, niwajuao. Na alipozungumza mambo kuhusu taifa hili, na ukomunisti, ingewatetemesha hata magotini mwenu, kweli, jinsi lilivyogubikwa. Hakuna kitu imara tena, si hata nchini mwetu wenyewe, hata kidogo.

93 Kuna kitu kimoja tu imara ninachojua kitasimama, hicho ni ule Mwamba, Yesu Kristo. Tunapokea ufalme ambao hauwezi kutikiswa. Na katika siku hii wakati kila kitu kinaanguka, tuna msingi imara, Bwana Yesu Kristo. Ingieni ndani Yake, marafiki. Ni kimbilio wakati wa dhoruba. Ni jambo la ajabu jinsi gani!

Aliona haya yote yakitimia.

94 Tunawaona Wayahudi sasa. Biblia ilisema ya kwamba Yerusalemu, nayo ingechanua kama waridi. Na jinsi wameimwagilia maji nchi hiyo! Na wao pia. . . Nabii alinena, akasema, "Siku ile," kwamba, "maji yatatoka kaskazini." Hakukuwako na maji huko wakati huo, hakuna chemchemi huko wakati huo. Lakini katika miaka michache iliyopita, kuna kisima kilichotokea, nacho kinamwagilia maji mabonde. Nao wanamwagilia; ni mojawapo ya maeneo makubwa zaidi ya kilimo, kwa ukubwa wake, duniani.

95 Na kemikali hizi zote kuu papo hapo kwenye Bahari ya Chumvi. Kuna kemikali za kutosha zilizopatikana chini yake, ambazo utajiri wote wa duniani haungeweza kuzinunua; kemikali, urani na chochote kile, chini kabisa ya Bahari ya Chumvi, ambayo sasa ni mali ya Israeli.

96 "Mtini ukichipusha majani yake." Isitoshe, bali miti mingine inachipusha majani yake. Wakomunisti wanachipusha majani yao. Mpinga-Kristo anachipusha majani yake.

97 Nalo Kanisa la Mungu linachipusha majani yake. Linachanua katika nguvu Zake tena. Tunutu amekula sehemu yake, parare amekula sehemu yake, tegu amekula sehemu yake, madumadu amekula sehemu yake, lakini Mungu alisema, "Utaishi tena." Anachanua majani yake sasa.

98 Miti inachipusha majani yake. Danieli aliliona hilo kimbele, akashangilia. Sasa, kwenye wakati huu, alisema, "Basi wakati huo . . ." Mlango wa 12.

> *Basi wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako: na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo . . . tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati . . . huo: na wakati huo watu wako wataokolewa, kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.*

99 Loo, jamani! Hivi huna furaha jina lako liko kwenye Kitabu Chake? Wakati yeye, Danieli, hapa, alipomwona, "Akija kwa Mzee wa siku, ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu. Naye akavifungua Vitabu. Nao wakahukumiwa, kila mtu, kwa hivyo Vitabu," ile hukumu kubwa ya Kiti Cheupe cha Enzi.

100 Sasa, Danieli anapewa hakikisho hili mwishoni mwa kipindi cha wakati wa Mataifa. Someni . . . mtakapoenda nyumbani, na kesho, someni mlango wa 11. Mnaweza kuona jinsi mfalme wa kaskazini anavyoshuka, ambaye si kitu kingine ila Urusi, ikishuka chini kuigandamiza, kama upepo wa kisulisuli. Navyo vile Vita vikuu vya Har-Magedoni vitapiganwa pale pale karibu na malango ya Yerusalemu. Angalieni. Loo, ninapenda hili!

> . . . *na wakati huo watu wako watakombolewa, kila mmoja* ambaye ameonekana *ameandikwa katika kitabu kile,* kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.

101 "Mikaeli, jemadari mkuu, atasimama upande wa" (akina nani?) "wa watu wako." Vema.

> *Na wengi wao walalao katika mavumbi ya ardhi wataamka* (lini?) nyakati hizi zitakapotimia, na *wengine kwa uzima wa milele, na wengine aibu na* kudharauliwa *milele.*

102 Hakika tu kama vile kulivyo na Uzima wa milele, kuna kuondolewa milele. Inategemea jinsi unavyomtendea Yesu Kristo katika maisha yako. Kama unampenda, na kuzaliwa mara ya pili, na unaye Roho Wake, unao Uzima wa milele. Kama humpendi, huna Uzima wa milele. Kama jina lako limeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, una Uzima usiopatikana na mauti. Ikiwa halijaandikwa Humo, hutatambulikana.

103 Ni kitu gani? Unabii huo wote unatimia; kila kitu, moja kwa moja hadi wakati huu.

104 Kichwa cha dhahabu kimepita, kama Danieli alivyosema kitapita, ufalme wa Babeli.

105 Kuufuatia huo, alisema, wangekuwa Wamedi na Waajemi. Waliufuata ufalme wa Babeli.

106 Nao wakaanguka, kwa (akina nani?) Wayunani, Aleksanda Mkuu.

107 Nao wakaanguka, kwa (akina nani?) Warumi. Nao Warumi wakavunjika, kwa ulimwengu wote, Rumi ya mashariki na ya magharibi, ile miguu miwili.

108 Naye alisema chuma na udongo ulikuwa juu ya vidole vya miguu, vile vidole kumi, falme kumi, naye akasema havitachanganyikana, nao wataoana wao kwa wao, Urumi na Uprotestanti.

109 "Na katika siku hiyo," wakati kitu hiki kikiwapo, "ndipo Jiwe likachongwa mlimani, bila kazi ya mikono, nalo likabingirika na kuvunja kitu hicho vipande-vipande." Nalo likachukua mahali pa ile sanamu.

110 Kwa hiyo, ndugu zangu, tuna matatizo, usiku wa leo. "Vita, matetesi ya vita; matetemeko ya nchi mahali mahali; hasira za wakati, shida nyingi kati ya mataifa." Nimerudi kutoka nchi za ng'ambo hivi punde tu, na sijaona taifa ambalo halitetemeki katika viatu vyao. Hawajui kitakachotukia baada ya hapa.

111 Lakini si tunashukuru, usiku wa leo, kwamba tunajua kitakachotukia baada ya hapa! Bwana Yesu Kristo atakuja mara ya pili, katika utukufu na ukuu! Na kila mwanamume au mwanamke atakayeonekana ameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, atafufuka pamoja na wapendwa wao, kumlaki Bwana hewani. Loo, ni jambo la ajabu jinsi gani! Ndiyo sababu tunasema:

> Tumaini letu halijajengwa juu ya kitu chochote
> Pungufu ya Damu ya Yesu pamoja na haki;
> Kila kitu karibu na nafsi yangu kikitoweka,
> Yeye ndiye tumaini na nanga yetu yote.

112 "Basi wakati huo, Mikaeli atasimama, mtawala mkuu." Mikaeli alikuwa Kristo, bila shaka, Yule aliyepiga vita vya Malaika Mbinguni, pamoja na ibilisi. Shetani na Mikaeli walipigana pamoja, ama walipigana mmoja na mwenzake, hasa.

113 Na, sasa, "Na kwenye wakati huo," alisema, "wote walioonekana wameandikwa katika Kitabu kile waliokolewa. Na wale waliotenda haki . . . " Tazameni hili.

> *Na walio na—na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na* kama . . .*na hao waongozao wengi kutenda haki kama nyota milele . . .*

114 Ninaangalia jambo hilo, wakati mwingine, na kuwazia, ndugu. Ninatoka nje, asubuhi. Ninapenda kuamka mapema. Je, hampendi kuamka mapema?

115 Nakumbuka wakati mimi na ndugu tulipokuwa milimani. Mapema sana asubuhi, yapata saa kumi, tungeamka. Tunaangalia, ikining'inia kule nyuma, na hiyo hapo ile nyota ya asubuhi. Kunaingia giza zito kabla tu ya mapambazuko.

116 Tunaona giza likikusanyika sasa. Ni kitu gani? Ni Nuru ikilisukuma giza. Moja halina budi kuondoka.

117 Vitu vyote vitambaavyo ambavyo vimekuwa vikipita mbio usiku kucha, jua hilo linapochomoza, hujificha mwanga unapomulika. Usiku na giza. . .Usiku na mwanga haviwezi kuwepo katika jengo moja. Ama ni giza au mwanga. Nao mwanga una nguvu kuliko giza.

118 Vivyo hivyo Kristo ana nguvu kushinda maadui wote wa ulimwenguni.

119 Sasa, tunafundishwa na wanasayansi; nuru inapoanza kuingia, inapunguza giza. Nalo giza linakusanya jeshi lake lote pamoja, kupigana na nuru, lakini nuru hushinda na kuingia.

120 Nayo Biblia ilisema, katika siku za mwisho, ya kwamba, "Shetani angeenda huku na huko kama simba angurumaye." Anawakusanya, leo, adui zake wote, marafiki zake wote, adui zetu, na kuwakusanya pamoja; wakilundikana chini ya kichwa kikubwa, ile alama ya mnyama, katika milki za kikanisa, muungano wa makanisa. Wote wakiungana na kujifanyia dhehebu kubwa, sawa na Ukatoliki.

121 Nazo milki za ulimwengu zinaungana pamoja, na kuunda kichwa kikubwa huko, katika milki za kisiasa, zinazoitwa ukomunisti.

122 Nayo Nuru ya Mungu inakaza mwendo. Ni nini kinatokea kwa wakati uo huo, kulifanya: Kanisa la Kikristo, Kanisa la Mungu aliye hai, linatiwa mafuta; nguvu zinalijia, linampokea Roho Mtakatifu.

123 Mwaka jana, katika milki za full Gospel, kulikuwa na waongofu milioni moja na laki tano. Ulio mkuu zaidi ulioenea nchini kwa miaka baada ya miaka. Hatuko uchochoroni tena. Tuko kwenye barabara pana ya haleluya. Hatuko kibandani, tena. Waongofu milioni moja na laki tano katika milki za full Gospel, mwaka jana, walipita Ukatoliki na lolote lingine. Loo, jamani!

124 Ni nini? Nuru inakusanyika. Ibada kuu za uponyaji zimeenea ulimwenguni kote. Haleluya! Huko ndani kabisa, huko Formosa, uamsho wa uponyaji unaendelea. Huko Japani, kampeni za uponyaji zinaendelea. Juu katika mikoa ya kaskazini yenye barafu, miamsho ya uponyaji inaendelea. Ulimwenguni kote, miamsho ya uponyaji! Haleluya! Wanadamu wanampokea Roho Mtakatifu, wa kila mahali. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

125 Inafanya nini? Ndipo ibilisi anasema, "Sasa ni wakati wangu." Anayakusanya majeshi yake. Muungano wa makanisa

unajaribu kuukomesha, ukisema, "Wao si kitu ila lundo la masanduku ya kelele. Hakuna kitu kwao. Yote ni ulokole. Hakuna kitu kama kutenda kazi katika milki za Kimbinguni."

126 Na wakati huo huo, mkuu wa Marekani...shirika la matibabu linaandika makala gazetini, kasema, "Hakuna mtu aliye na haki ya kuingia kwenye chumba cha wagonjwa, kuwahudumia watu, asiyemwamini Mwenyezi Mungu na kumkubali kama Msaidizi wake." *Mbiu Ya Mkristo,* likiwahoji madaktari mwezi uliopita, liliandika makala nisiyoweza kuandika, mimi mwenyewe, iwapo nilikuwa nikijaribu kujisifu juu yake. Ni nini? Katikati ya kila kitu, Mungu atasababisha adui Zake kushuhudia kwa utukufu Wake. Naam, bwana. Huyo daktari alisema, "Tunaweza tu kutoa misaada, lakini Mungu ndiye mponyaji."

Nikasema, "Hao wataalamu wakuu wameanza tu kujua kile ambacho sisi kundi la wapumbavu tumejua sikuzote." Hiyo ni kweli.

127 Baadhi ya siku hizi tukufu, utagundua ya kwamba kundi hili la Nguvu, linalowabadilisha makahaba wakawa wanawake wenye heshima, na walevi wakawa waungwana na Wakristo, ndizo Nguvu zile zile zitakazowainua watoke humu duniani na kuwapeleka Nyumbani katika Unyakuo, Utukufuni. Huenda imechelewa sana; huenda imechelewa sana kwa wengi.

128 "Siku hiyo, Mikaeli atasimama upande wa watu." Hasimamii mataifa. Anasimama upande wa watu. "Na wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi, wengine watafufuka wapate aibu na kudharauliwa milele. Bali walio na hekima na wawaongozao wengi kutenda haki, watang'aa kama nyota milele na milele." Haleluya!

> Hema au nyumba ndogo, kwa nini nijali?
> Wananijengea ikulu Kule! (Njoni mkanitembelee siku moja!)

129 Ni nini? Nimetembea na kuitazama nyota hiyo kuu ya asubuhi, inapoanza kusogea huko nga'mbo. Je, nyota ya asubuhi inasema nini? Nyota ya asubuhi inaakisi tu nuru kuu ya jua linalokuja. Hiyo ni kweli? Nyota ya asubuhi, sababu ya kuwa yenye kung'aa sana hivi (mnajua ni kwa nini?), jua liko karibu nayo zaidi sana. Linasukuma. Nayo nyota ya asubuhi inakukaribisha kuja kwa jua.

130 Vema, enyi nyota za asubuhi, wakati wa kuanza kumkaribisha Yeye akija umewadia! Angazeni, enyi Nyota za asubuhi! Amkeni mapema! Inasema, "Mwana atakuwa hapa hivi karibuni!"

131 Tunapotazama na kuiona ile nyota ya asubuhi, ikimetameta angani, ina maana kwamba jua litawaka hivi karibuni sana.

132 Basi tunapoziona Nyota za asubuhi za Mungu, zikisimana na kuangaza kwa utukufu wa kufufuka kwa Yesu Kristo, inaonyesha kwamba yule aliye Mkuu anakaza mwendo. Taa zinakusanyika, lakini Nyota ya asubuhi inapiga kelele, "Shikilia! Sio muda mrefu hadi mapambazuko." Shikilia! Si muda mrefu hadi mapambazuko. Endelea tu kushikilia. Kama vile Dada Murphy na hao wengine walivyozoea kuimba, "Endelea tu kushikilia; mchana unakuja hivi karibuni." Shikilieni kwake! Nyota za asubuhi zinauangazia ulimwengu sasa, kuuangazia ulimwengu, kabla tu ya lile giza kuu, pamoja na ile radi kuu kutoka Mbinguni, kule Kuja kwa Bwana.

Sikilizeni kwa makini sasa. Sasa alisema . . .

133 Nimeitazama nyota ya asubuhi, nikawaza, "Loo, nyota ya asubuhi!" Nikatazama chini . . .

134 Siku moja, tukisimama huko juu, mimi pamoja na Ndugu Wood. Alikuwa ndio kwanza awashe moto, nasi tulikuwa tunaenda kula kiamshakinywa. Ndipo nikageuka na kuitazama ile nyota ya asubuhi. Nikatembea huko kwenye vichaka vya mierezi; huku pepo zinanong'oneza kupitia misonobari. Nikasimama kule. Nilijisikia vizuri, nikipumua hewa hiyo nzuri, safi ya asubuhi; na kidogo ni baridi, baridi sana. Nikashuka mpaka kwenye kijito, nikachota ndoo ya maji, yanaganda kabla hujapanda juu.

135 Nikisimama huko juu, nikiinua mikono yangu, huko nje kwenye misonobari hiyo. Niliitazama nyota ya asubuhi. Nikawazia, "Loo, angalieni hapa, vile miaka arobaini na mitano imenifanyia." Nikasema, "Loo, angalieni hapa. Ninazidi kuingia makunyanzi. Mikono yangu inaingia makunyanzi; nywele zinaanguka; meno yanatoka. Loo, yale miaka arobaini na mitano imenifanyia! Lakini," nikasema, "angalia huko ng'ambo, nyota ile ya asubuhi ni nzuri na yenye kung'aa kadiri ilivyokuwa siku ambayo Mungu, 'whiu,' alipoipeperushia mikononi Mwake, na kusema, 'Na iangaze!'"

136 Kisha nikafikiria juu ya Maandiko haya. Nikasema, "Lakini Mungu aliahidi, kama tutakuwa na hekima na kuwaongoza wengi kutenda haki, tutang'aa kuliko nyota milele."

137 Nikawazia, "Nyota ya asubuhi, unang'aa sasa, lakini ngoja hata tutakapofika Huko! Haleluya! 'Tutang'aa kuliko nyota milele!'"

138 Nami ningeweza kusikia upepo ule ukishuka kilimani, karibu tu na mapambazuko ya mchana, ukinong'oneza kupitia misonobari hiyo, ukisema:

Kuna Nchi iliyo ng'ambo ya mto,
Tunayoiita tamu milele,

Nasi tunafikia tu ufuko huo kwa hatua ya imani;
Mmoja mmoja twaingia langoni,
Huko tukaishi pamoja na wasiopatikana na mauti,
Watakapopiga kengele hizo za dhahabu kwa ajili yangu na yako.

139 Ni jambo kuu jinsi gani! "Walio na hekima watawaongoza wengi kutenda haki, nao watang'aa kuliko nyota milele na milele."

140 Kwa hivyo inaleta tofauti gani, kwa vyovyote vile? Maskini kipindi hiki kidogo cha wakati hapa ni cha nini? Maskini vumbi hili la ardhi, mdudu asiye na uti wa mgongo, maskini mwili unaopatikana na mauti ambao hauna budi kuharibika na kurudi mavumbini, nao mabuu ya ngozi wataula! Loo, jamani! Jalia niamke pamoja na yote yaliyo ndani yangu, na kuangaza kwa ajili ya utukufu wa Mungu! Weka kando kila mzigo, ili Roho Mtakatifu aweze kupitisha nguvu na utukufu Wake, kwa kuhubiri Injili na uponyaji wa wagonjwa, kumthibitisha Yesu Kristo aliyefufuka katika wafu. Loo, jamani!

. . .*milele na milele.*

Lakini ewe,. . .Danieli, yafunge maneno haya, ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho: kwa maana *wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa* yataongezeka.

Ndipo mimi Danieli, nikatazama na *kuangalia, na kumbe, wamesimama wengine wawili, mmoja ukingoni mwa mto upande huu, na* mmoja *ukingoni. . .ukingoni mwa mto upande wa pili.*

Na mmoja akamwuliza yule mtu aliyevikwa nguo za kitani (Roho Mtakatifu), *aliyekuwa juu ya maji* (watu na makutano). . .

141 Roho Mtakatifu juu ya watu! Loo! Haleluya! Roho Mtakatifu!

142 Ufunuo :15, :16, inasema kwamba jamaa na makutano. . . *maji* yanamaanisha "jamaa na umati wa watu."

143 "Na Huyu hapa aliyevikwa nguo za kitani nyeupe, akielea huko na huko, juu ya maji, huku ameinua mkono Wake kuelekea Mbinguni, akiapa kwake Yeye aliye hai milele na milele, 'Mambo haya yatakapotokea, hakutakuwa na wakati baada ya haya!'" Haleluya!

144 "Hakutakuwa na wakati baada ya haya!" Aliapa ya kwamba, tutakapoyaona mataifa haya yakivunjika, na mambo yakitukia namna hiyo, "Siri ya Mungu tayari imetimia."

145 Ni nini, "Siri ya Mungu"? "Mungu ndani yako, tumaini la Utukufu," akiangaza, ubatizo wa Roho Mtakatifu!

146 Kisha akasema, “Mambo haya yatakapotukia, hakutakuwa na wakati baada ya haya.”

147 “Wale wamjuao Mungu wao,” alisema Danieli. “Katika siku za mwisho, wengi wataenda mbio huko na huko, maarifa yataongezeka. Lakini wale wamjuao Mungu wao watatenda mambo makuu katika siku za mwisho.”

148 “Watatenda mambo makuu.” Loo, matendo makuu ya imani yanatokea, kote ulimwenguni, usiku wa leo, tena na tena. Kote katika mataifa, miamsho mikuu! Vipofu wanaona. Viziwi wanasikia. Viwete wanatembea. Watu wa matabaka yote ya maisha wanaingia. Wanampokea Roho Mtakatifu; si maskini na ombaomba tu, bali mamilionea na wengine wote. Mungu anachukua na kuweka vazi Lake juu ya kila mmoja, na kuwapa mwaliko kwenye Karamu ya Arusi.

149 Naye Kuhani Mkuu, Melkisedeki, atakuja siku moja. Nasi tutakula ushirika, upya, pamoja Naye, katika Ufalme wa Mungu, mojawapo ya siku hizi kuu, tukufu! Loo, nina furaha sana, usiku wa leo, kuwa katika Ufalme Wake! Naam, bwana. Siku fulani kuu, nzuri, siku nzuri sana, “Hakutakuwa na wakati tena!”

150 Mnaona, tulitoka katika Umilele. Tulikuwako, kabla ulimwengu haujakuwapo. Je, ulijua hilo? Mungu alimuumba mtu kwa sura Yake Mwenyewe.

151 “Ulikuwa wapi,” alimwambia Ayubu, wakati Ayubu alipodhania alikuwa na hekima. Kasema, “Ulikuwa wapi nilipoweka msingi wa ulimwengu, kabla sijauweka, hapo wana wa Mungu walipoimba pamoja, na nyota za asubuhi zikapaza sauti kwa furaha?”

152 “Nyota za asubuhi zilipaza sauti kwa furaha.” Hao wenye kung’aa walipaza sauti kwa furaha, walipoona ya kwamba siku moja walikuwa wamekaa kwenye maskani hapa duniani. Naye Mfalme, Melkisedeki, angekuja katika haki ya Mungu, na kuutoa uhai Wake, apate kutukomboa kwa Mungu, kurudi tena, na kung’aa kuliko nyota milele na milele.

153 “Ulikuwa wapi nilipoweka msingi wa dunia? Tangaza mahali imeshikizwa. Niambie inakosimamia.” Kasema, “Jifunge mshipi. Nataka kuongea na wewe kama mwanaume.” Ndipo Ayubu akaanguka kifudifudi kama mtu aliyekufa. Asingeweza kustahimili. Mungu alikuwa hapo. Haya basi. “Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya ulimwengu?”

154 Injili hii tukufu imetabiriwa na manabii wa Agano la Kale. Imeshuka kupitia nyakati. Iko hapa usiku wa leo. Imethibitishwa na Mungu. Imeenea ulimwenguni. Wamejaribu kuizima.

155 Lakini, hebu jaribu kuuzima moto siku yenye upepo, na mba—na mbao kavu mbele yake. Mbona, huwezi kufanya hivyo. Kadiri unavyopigana nao, ndivyo unavyozidi kuupulizia upepo;

kadiri unavyoupulizia upepo mwingi, ndivyo utakavyowaka kwa nguvu zaidi. Hilo ndilo jambo pekee.

156 Tulizoea kuwa na moto mdogo, huko milimani, nilipokuwa nikijaribu kuuwasha moto asubuhi na mapema. Ningetoka pale na kuutupia vijiti; ukaanza kutoa moshi. Najua, maadamu kuna moshi kidogo, kuna moto pale mahali fulani. Kitu pekee nilichopaswa kufanya ni kuchukua kofia yangu na kuanza kuupepeta, na hatimaye ukawaka.

157 Hicho ndicho Kanisa linachohitaji leo hii, ni kupepetwa tena kwa Upepo wenye nguvu ukienda kasi kama ulivyoshuka katika Siku ya Pentekoste, kulipepeta lipate kuirudia Imani tena, kumpokea Bwana Yesu Kristo wakati wa kuja Kwake katika Utukufu.

158 Angalieni ishara, maajabu, mambo ya kisiri yanayotokea. "Matetemeko ya nchi mahali mahali; mawimbi makubwa yakitokea ukingoni," kama vile Yesu alivyosema yangetokea, "mioyo ya watu ikizimia; hofu."

159 Hofu, "Loo, ni nani atakayerusha bomu la kwanza la kobalti? Itakuwaje? Katika saa chache ulimwengu wote utaangamizwa." Mbona, tungekuwa Mbele za Mungu kabla hata halijarushwa kutoka kwenye ndege. Hiyo ni kweli. Itakuwaje? Hakutakuwa na chochote, lakini tutaangusha . . .

> Maskini vazi hili la mwili tutaliangusha, na kuinuka
> Na kutwaa tuzo la milele,
> Na kupiga makelele, wakati tukipitia hewani,
> "Kwaheri, kwaheri, saa tamu ya maombi!"

160 Yote yatakwisha, nasi tutaenda Nyumbani. Tuulaze mwili huu wa kale chini; tuubadilishe kwa taji na joho, huko ng'ambo, ambalo halitafifia. Kugeuka kutoka kwa mzee, mwanamke mzee, kuwa kijana, wapate kuishi milele na milele, tuangaze zaidi; na kutopatikana na mauti, kutembea huku na huko kwenye mitaa ya Utukufuni, Uweponi mwa Bwana Yesu Kristo. Waliimba, "Utukufu kwa Mungu aliye Juu! Amefanya mambo makuu miongoni mwetu."

161 Tukiwa safarini leo, huku Nguvu za Mungu zikithibitisha kila jambo pande zote, hebu tuangalie pande zote tuone mahali tulipo. Tuutazame mtini ukichipusha majani yake. Tuitazame miti hiyo mingine inayochipusha majani yake. Tuyatazame mataifa yakichipusha majani yake. Tuliangalie Kanisa la Roho Mtakatifu likichipusha majani yake. Tuitazame Pentekoste ikijirudia, ikirudi, ishara zile zile na maajabu. Haleluya!

Na tuombe.

162 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe usiku wa leo, kwa ajili ya Nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo, kwa Utu Wake mkuu, kwa upako Wake wa Roho Mtakatifu. Tunakushukuru

Wewe kwa sababu Yeye yuko hapa sasa, yu hai, yu hai daima, akifanya maombezi juu ya maungamo yetu. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya Nguvu Zake za uponyaji zilizotunyakua kama vijinga vya moto, Bwana, zikatutoa kaburini, zikatuinua na kufanya upya nguvu zetu, na kutupa Nguvu, tupate kuondoka na kuangaza humu katika giza hili. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili.

163 Baba, tunaomba ya kwamba utambariki kila mtu ambaye hajaokoka. Wabariki wote waliookoka. Tujalie, Baba. Waponye wagonjwa wote; upate utukufu. Ibariki maskani hii ndogo. Wabariki hawa watu. Mbariki Ndugu Neville, mchungaji. Wabariki mashemasi wote, wadhamini. Tujalie, Bwana. Weka mikono Yako ya uponyaji juu yao. Na kama ibilisi akiingia na kusababisha tofauti ndogo ndogo, ziponye, Bwana, upesi sana, kwa Zeri ya Gileadi. Tujalie, Bwana. Mimina mafuta ya kupaka juu yao. Wafanye wanyenyekevu moyoni, watamu nafsini. Jalia watembee katika nyayo za Bwana Yesu. Mambo ya kimwili huwapata, nao wanakuwa wagonjwa, naomba Malaika wa Mungu asimame karibu, kuweka Damu ya Yesu. Tujalie. Ponya maradhi yote.

164 Nisaidie, Bwana, ninapotoka kwenda hudumani, nikiona haja hizo kuu. Ni haja iliyoje katika siku hii! Mamilioni wamekufa. Wapagani mia moja arobaini na nne elfu walikufa leo, bila kumjua Kristo. Nisaidie, Mungu Mpendwa. Tubariki sisi sote, pamoja.

165 Na siku moja, utufufue kutoka humu duniani, huko ng’ambo, Bwana, kuketi pamoja na Wewe katika kiti Chako cha enzi, katika mahali pa Mbinguni kule juu, katika Kristo Yesu. Tujalie, Baba. Hadi wakati huo, afya na nguvu ziwe zetu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Loo, nataka kumwona Yeye, nataka kuutazama uso Wake,
Huko nikaimbe Milele juu ya neema Yake iokoayo.
Kwenye mitaa ya Utukufuni nijalie nikainue sauti yangu;
Masumbuko yote yamepita, hatimaye niko Nyumbani, kushangilia milele.

Nisafiripo kwenye nchi hii, nikiimba safarini,
Nikizielekeza nafsi Kalvari, kwenye mtiririko mwekundu,
Mishale mingi huchoma nafsi yangu kutoka nje, ndani;
Lakini Bwana wangu huniongoza, sina budi kushinda Kwake.

Loo, nataka kumwona Yeye, niutazame uso Wake,
Huko nikaimbe Milele juu ya neema Yake iokoayo.
Kwenye mitaa ya Utukufuni nijalie niinue sauti yangu;
Masumbuko yote yamepita, hatimaye niko Nyumbani, kushangilia milele.

166 Sasa sikilizeni, kidogo tu. Ni Wamethodisti wangapi walio hapa? Inueni mikono yenu. Wamethodisti? Ni Wabaptisti wangapi walio hapa? Inueni mikono yenu. Je, ni Wapresbiteri wangapi hapa? Inueni mikono yenu. Wanazarayo wangapi? Inueni mikono yenu. Wapentekoste wangapi? Inueni mikono yenu. Walutheri wangapi? Inueni mikono yenu. Vema, sote tuko hapa. Tazameni, kundi kubwa mno, lililochanganyikana, wote wameketi mahali pamoja, katika mahali pa Mbinguni, wakizifurahia zile Baraka.

167 Sasa ninataka Wamethodisti wapeane mikono na Wabaptisti, Wabaptisti na Walutheri. Geukeni sasa na kupeana mikono, kisha geukeni nyuma hivi, sasa, tunapouimba.

Nikielekeza nafsi Kalvari, kwenye mtiririko mwekundu,
Mishale mingi huichoma nafsi yangu kutoka nje, ndani;
Lakini Bwana wangu huniongoza, sina budi kushinda Kwake.

Loo, nataka kumwona Yeye, niutazame uso Wake,
Huko nikaimbe milele juu ya neema Yake iokoayo.
Kwenye mitaa ya Utukufuni nijalie nikainue sauti yangu;
Masumbuko yote yamepita, hatimaye niko nyumbani, kushangilia milele.

168 Je, huo hauwafanyi kujisikia vizuri? Hivi hauwafanyi kujisikia kama ninii yenu yote . . . ? Ni Wakristo wangapi waliopo hapa? Inua mkono wako. Kila mtu anayemwamini Bwana Yesu Kristo, inua mkono wako. Loo, jamani! Ni jambo la ajabu jinsi gani!

169 Sasa tunapotengana, tunapoenda, kutoka kwenye makazi yetu mbalimbali, hebu twendeni kwa maombi. Sasa hebu tuuimbe wimbo wetu mzuri, wa kale wa kufumukana. Ni wangapi wanaoujua? *Peleka Jina La Yesu*. Kila mtu pamoja sasa, hebu tuimbe.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na wa majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Lipeleke, kila uendako.

Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu! (Loo jinsi lilivyo tamu!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
(Naam, Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Sikilizeni:

Tukiliinamia Jina la Yesu,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,
Loo, wakati safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu! (Loo jinsi lilivyo tamu!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

170 Hiki hapa ninachotaka mfanye.

Peleka Jina la Yesu,
Kama Ngao dhidi ya kila adui;
Wakati majaribu yanapokuzunguka,
Taja Jina hilo Takatifu katika maombi.

Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Mwanzo Na Mwisho Wa Kipindi Cha Mataifa SWA55-0109E
(Beginning And Ending Of The Gentile Dispensation)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 9 Januari, 1955, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org